PAN-AFRICAN PARLIAMENT

البرلمان الأفريقي

PARLEMENT PANAFRICAIN

PARLAMENTO PAN-AFRICANO

Ref: PAP.5/PLN/RECOMS/X-Y/OCT.19
Asili: Kifaransa

# BUNGE LA TANO

# MKUTANO WA TATU WA KAWAIDA

# KUANZIA TAREHE 6 HADI 18 OKTOBA 2019

# MAPENDEKEZO

*Kaulimbiu ya mwaka 2019: "Mwaka wa Wakimbizi, Wanaorejea makwao na Wakimbizi wa Ndani: Mchango wa Bunge la Afrika Kuelekea Kupata Suluhisho la Kudumu la Uhamiaji wa kulazimishwa barani Afrika"*

Gallagher Convention Centre, Private Bag X16, Midrand 1685, Johannesburg, Republic of South Africa
Tel: (+27) 11 545 5000 - Fax: (+27) 11 545 5136 – Website: www.panafricanparliament.org
Email: secretariat@panafricanparliament.org

## PENDEKEZO KUHUSU UPATIKANAJI WA NISHATI KWA WOTE

**BUNGE LA AFRIKA,**

**LIKIZINGATIA** Ibara ya 17 (1) ya Mkataba Ulioanzisha Umoja wa Afrika ambao ulianzisha Bunge la Afrika ili kuhakikisha ushiriki kamili wa watu wa Afrika katika maendeleo na ushirikiano wa kiuchumi wa bara;

**LIKINGATIA PIA** Ibara ya 3 ya Mkataba Ulioanzisha Umoja wa Afrika, ambapo malengo yake, pamoja na mambo mengine, ni kuharakisha muungano wa kisiasa, kijamii na kiuchumi wa bara la Afrika; kukuza ushirikiano wa kimataifa, kwa kuzingatia Mkataba wa Umoja wa Mataifa na Azimio la Dunia la Haki za Binadamu; kuhamasisha maendeleo endelevu kwenye masuala ya kiuchumi, kijamii na kiutamaduni, na pia kuunganisha uchumi wa Afrika; kuratibu na kuoanisha sera miongoni mwa jumuiya za uchumi za kanda zilizopo na za siku za baadaye kwa lengo la kufikia hatua kwa hatua malengo ya Umoja wa Afrika;

**LIKIZINGATIA PIA** Ibara ya 3 ya Protokali ya Mkataba ulioanzisha Jumuiya ya Uchumi ya Kanda inayohusiana na Bunge la Afrika na ibara ya 4 (a) ya Kanuni za Undeshaji wa Bunge la Afrika ;

**LIKIZINGATIA** umuhimu wa nishati kwenye ukuaji jumuishi kwa ajili ya maendeleo ya Afrika;

**LIKIZINGATIA PIA** kiwango cha chini cha uwekezaji katika sekta ya nishati katika nchi nyingi za Afrika;

**LIKIZINGATIA PIA** kutokuwepo kwa sera thabiti ya nishati pamoja na kutokuwepo kwa mfumo wa kisheria barani Afrika;

**LIKIAMINI** kuna haja ya kutekeleza programu za UNIDO kuhusu maendeleo ya viwanda barani Afrika;

**KWA MUJIBU WA** Ibara ya 5 al. D ya Kanuni za Uendeshaji wa Bunge la Afrika, ambayo inalipa mamlaka ya kutoa mapendekezo na maazimio kuhusu masuala yote yanayohusiana na Umoja wa Afrika na vyombo vyake, Jumuiya za Uchumi za Kanda na vyombo vyao, kwa Nchi wanachama na vyombo na taasisi zao;

**SASA LINAAZIMIA:**

1. Kutangaza upatikanaji wa nishati kwa wote kwa bei nafuu na mabadiliko kwenye sekta ya nishati na kuhakikisha upatikanaji wa nishati mbadala kwa wote ifikapo mwaka 2040;

2. Kutoa mafunzo kwa rasilimali watu katika ngazi ya chini kuhusiana na masuala ya nishati na kusaidia maendeleo yao, kuwaelimisha wananchi kuhusu umuhimu wa nishati mbadala;

3. Kuhimiza nchi wanachama kutumia sehemu kubwa ya bajeti zao kwa ajili ya nishati mbadala;

4. Kuanzisha utaratibu wa kukusanya fedha kwa ajili ya nishati mbadala;

5. Kutoa misamaha ya ushuru kwa vifaa vinavyotumia nishati mbadala;

6. Kuanzisha sera madhubuti ya nishati katika nchi za Afrika;

7. Kuhimiza na kusaidia mipango ya nishati ya kikanda;

8. Kuhimiza uwekezaji wowote unaohusiana na nishati mbadala;

9. Kusisitiza umuhimu wa utekelezaji mzuri wa lengo namba 05 la Malengo ya Maendeleo Endelevu (kuweka usawa wa kijinsia na kuwawezesha wanawake na wasichana wote);

10. Kuhimiza ubia kati ya sekta ya umma na binafsi katika uwekezaji kwenye nishati;

11. Kuanzisha mtandao wa wabunge unaohusika na matumizi ya nishati mbadala;

12. Kuandaa sheria ya mfano ya nishati mbadala.

**Limepitishwa Midrand, Afrika Kusini**

**Tarehe 17 Oktoba 2019**

# PENDEKEZO KUHUSU WAJIBU WA KIJAMII WA WABUNGE KATIKA MAPAMBANO DHIDI YA AJIRA KWA WATOTO WALIO KATIKA MAENEO YA MIGODI

**BUNGE LA AFRIKA,**

**LIKIZINGATIA** Ibara ya 17 (1) ya Mkataba Ulioanzisha Umoja wa Afrika ambao ulianzisha Bunge la Afrika ili kuhakikisha ushiriki kamili wa watu wa Afrika katika maendeleo na ushirikiano wa kiuchumi wa bara;

**LIKIZINGATIA PIA** Ibara ya 3 ya Protokali ya Mkataba ulioanzisha Jumuiya ya Uchumi ya Kanda inayohusiana na Bunge la Afrika na ibara ya 4 (a) ya Kanuni za Undeshaji wa Bunge la Afrika ;

**LIKIZINGATIA PIA**, vifungu vya Mkataba wa Umoja wa Mataifa kuhusu Haki za Mtoto na Mkataba wa Afrika kuhusu Haki na Ustawi wa Mtoto, ambapo nchi nyingi za Afrika zimeridhia na kuingiza katika sheria zao, hususani kwa kupiga marufuku ajira kwa watoto;

**LIKIZINGATIA** mahitimisho ya Ripoti ya ziara ya kutafuta ukweli wa mambo kuhusu wajibu wa wabunge katika mapambano dhidi ya ajira kwa watoto katika maeneo ya migodi, iliyofanywa na Kamati ya Afya, Kazi na Masuala ya Kijamii, kuanzia tarehe 16 hadi 18 Septemba, 2019 huko Abidjan, Ivory Coast;

**LIKITAMBUA PIA** kwamba Sekta ya madini ni moja ya sekta muhimu zaidi barani Afrika, lakini iko kwenye orodha ya shughuli hatari zaidi ulimwenguni, hususani kwa watoto;

**LIKISIKITISHWA** na unyonyaji wa watoto katika shughuli za kiuchumi ambazo huwasababishia unyanyasaji wa aina mbalimbali na hatari kubwa ya kudhoofika kwa afya na ukuaji wao;

**LIKISIKITISHWA ZAIDI** na takwimu kubwa zinazooneshwa na utafiti wa UNICEF wa mwaka 2016 ambapo zinaonesha kwamba huko Ivory Coast, kazi hatarishi zinaathiri watoto 1,622,140 kati ya 2,213,708 wanaofanya shughuli za kiuchumi, au sawa na asilimia 73.3 ya watoto .

**LIKITAMBUA** kwamba sekta ya kilimo inaajiri watoto wengi zaidi takribani asilimia 56.2, sekta ya huduma asilimia 41.9, asilimia 21.5 ya watoto wenye umri wa miaka kati ya 5 na 7 nchini Ivory Coast wanafanya kazi hatarishi hususani uvunjaji na usafirishaji mawe, upasuaji wa miamba kwa kutumia baruti, kazi za chini ya ardhi, uchimbaji na usafishaji wa dhahabu kwa kutumia zebaki na cyanide ;

**LIKIPONGEZA** juhudi za Umoja wa Afrika za kuimarisha ulinzi wa haki za watoto kupitia uandaaji wa Mpango Kazi wa Miaka Kumi unaohusiana na kukomesha ajira kwa

watoto, ajira za shuruti na utumwa mamboleo na usafirishaji haramu wa binadamu barani Afrika;

**LIKIPONGEZA PIA** juhudi za Ivory Coast kwa kuimarisha sera zake za ajira kwa watoto, hususan kupitia Azimio la Mpango wa Pamoja wa mwaka 2010 lenye lengo la kusaidia utekelezaji wa Protokali ya Harkin-Engel; kusainiwa kwa Makubaliano ya Ushirikiano katika eneo la Afrika Magharibi pamoja na Ghana na Burkina Faso; uundaji wa kamati ya kitaifa inayohusisha wizara mbali mbali (CIM) na Kamati ya Usimamizi ya Kitaifa (CNS) pamoja na kupitishwa kwa sera za kitaifa, hususan mpango kazi wa 2019-2021 wa kupambana na ajira kwa watoto;

**LIKIRIDHISHWA** na maandalizi yote yaliyofanywa na Ivory Coast kwa ajili ya kuwezesha ziara ya ujumbe wa BA na **LIKIPONGEZA** ushirikiano kati ya wabunge, wawakilishi wa wizara mbalimbali na asasi za kiraia za Ivory Coast ambao wameunga mkono juhudi za Wabunge wa Bunge la Afrika kwa kuwapa data na habari za kuaminika,

**LIKIKUMBUSHA** kwamba nchi wanachama zina jukumu la kutoa hifadhi ya jamii kwa wananchi kwa kuweka mazingira wezeshi ili kuwawezesha kupata mahitaji ya msingi kama elimu, maji, nyumba na huduma za afya;

**SASA LINAAZIMIA:**

1. **Kwa** nchi wanachama :
   - **i.** **KUKUZA** na **KULINDA** haki za binadamu, hususan zile za makundi yaliyo katika mazingira hatarishi kama watoto kupitia uimarishaji wa mifumo ya kitaifa ya kulinda haki hizi.
   - **ii.** **KUUNDA** au, ikibidi, **KUFUFUA** mabunge ya watoto kama jukwaa linalowawezesha kushughulikia na kutatua matatizo yao kwa njia nzuri;

2. Kwa Wabunge wa nchi wanachama **KUTUMIA** kikamilifu mamlaka yao ya kusimamia shughuli za serikali na **KUPITISHA** sheria husika na kuhakikisha zinatekelezwa kikamilifu huku kukiwa na adhabu dhidi ya wale wanaokiuka sheria hizo.

3. Kwa Kamati ya Afya, Kazi na Masuala ya Kijamii kufanya mashauriano ya kikanda kuhusu utumikishaji wa watoto kwa lengo la kuimarisha mafanikio yao kwenye ulinzi wa haki zao.

Limepitishwa Midrand, Afrika Kusini

Tarehe 17 Oktoba 2019

**PENDEKEZO KUHUSU KURIDHIA MKATABA WA KUJENGA UWEZO WA AFRIKA WA KUKABILIANA NA MAJANGA**

**BUNGE LA AFRIKA,**

**LIKIZINGATIA** Ibara ya 17 (1) ya Mkataba Anzilishi wa Umoja wa Afrika ambao ulianzisha Bunge la Afrika ili kuhakikisha ushiriki kamili wa watu wa Afrika katika maendeleo na ushirikiano wa kiuchumi wa bara;

**LIKINGATIA PIA** Ibara ya 3 ya Protokali ya Mkataba unaoanzisha Jumuiya ya Uchumi ya Afrika inayohusiana na Bunge la Afrika, Kanuni ya 4(a) ya Kanuni za Uendeshaji za Bunge la Afrika

**LIKISHAWISHIKA** kwamba Taasisi ya Kujenga Uwezo wa Afrika wa Kukabiliana na Majanga ina jukumu kubwa kwenye kujenga ustamihilivu wa kifedha ili kukabiliana na majanga yanayotokanan na mabadiliko makubwa ya tabianchi na majanga mengine barani Afrika, kupitia utoaji wa msaada wa kitaalamu kwa nchi za Afrika na kuandaa huduma nyingine zenye ubunifu za bima ili kukabiliana na majanga;

**LIKISHAWISHIKA ZAIDI** kwamba Taasisi ya Kujenga Uwezo wa Afrika wa Kukabiliana na Majanga inachangia kwenye lengo la Ajenda 2063 la kujenga ustamihilivu wa bara la Afrika dhidi ya majanga yatokanayo na mabadiliko ya tabianchi ili kuimarisha utayari wa kifedha ili kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi na hivyo kuchangia kulinda jamii zilizo kwenye mazingira hatarishi na kulinda faida zinazotokana na maendeleo;

**LIKIZINGATIA** wasilisho kuhusu Mkataba wa Kujenga Uwezo wa Afrika wa Kukabiliana na Majanga lililofanywa kwenye Mkutano wa Tatu wa Kawaida wa Bunge la Tano la Bunge la Afrika tarehe 16 Oktoba 2019;

**LIKISIKITISHWA SANA** na kasi ndogo ya kuridhia Mkataba wa Kujenga Uwezo wa Afrika wa Kukabiliana na Majanga ambapo kati nchi 33 zilizopaswa kusaini Mkataba huo, ni nchi 8 pekee zilizoridhia;

**KWA MUJIBU wa** Kanuni ya 5(d) ya Kanuni za Uendeshaji wa Bunge la Afrika, ambayo inalipa BA madaraka ya kutoa mapendekezo na kuweka maazimio kuhusu jambo lolote linalohusiana na Umoja wa Afrika na vyombo vyake, Jumuiya za Uchumi za Kanda, Nchi Wanachama na vyombo na taasisi zake;

HIVYO LINAPENDEKEZA:

1. Nchi wanachama wa Umoja wa Afrika ambazo hazijasaini na kuridhia Mkataba wa Kujenga Uwezo wa Afrika wa Kukabiliana na Majanga kuharakisha michakato yao ya kusaini na kuridhia Mkataba huo;

2. Mabunge ya Kitaifa kuendelea kushawishi uharakishaji wa michakato ya kuridhia Mkataba wa Kujenga Uwezo wa Afrika wa Kukabiliana na Majanga ;

3. Nchi wanachama wa Umoja wa Afrika kuthibitisha dhamira zao kwenye dira ya mwanzo iliyosababisha kuanzishwa kwa Taasisi ya Kujenga Uwezo wa Afrika wa Kukabiliana na Majanga kama suluhisho la kiafrika kwa matatizo ya Afrika yanayosababishwa na mabadiliko ya tabianchi, kupitia msaada na ushiriki kamili katika mfumo wa pamoja wa kukabiliana na majanga barani Afrika;

4. Taarifa kuhusu Taasisi ya Kujenga Uwezo wa Afrika wa Kukabiliana na Majanga inabidi zitolewe mara kwa mara kwa Kamati ya Uchumi Vijijini, Kilimo, Mazingira na Maliasili ya Bunge la Afrika kuhusu shughuli zake na hali ya kuridhia;

5. Taasisi ya Kujenga Uwezo wa Afrika wa Kukabiliana na Majanga ilisaidie Bunge la Afrika kuandaa mfumo utakaoongoza ushirikiano wa Mabunge ya Kitaifa katika kufuatilia na kutathmini maendeleo ya kuridhia, kutumika ndani ya nchi na utekelezaji wa Mkataba wa Kujenga Uwezo wa Afrika wa Kukabiliana na Majanga

**Limepitishwa Midrand, Afrika Kusini**
**Tarehe 17 Oktoba 2019**

**PENDEKEZO KUHUSU RIPOTI YA MWISHO YA KAMATI YA UKAGUZI NA HESABU ZA UMMA YA BUNGE LA AFRIKA**

**BUNGE LA AFRIKA**,

**LIKIZINGATIA** Ibara ya 17 (1) ya Mkataba Anzilishi wa Umoja wa Afrika ambao ulianzisha Bunge la Afrika ili kuhakikisha ushiriki kamili wa watu wa Afrika katika maendeleo na ushirikiano wa kiuchumi wa bara;

**LIKIZINGATIA** Ibara ya 3 ya Protokali ya Mkataba uliyoanzisha Jumuiya ya Uchumi ya Kanda inayohusiana na Bunge la Afrika, na Kanuni ya 4(a) ya Kanuni za Uendeshaji wa Bunge la Afrika, inayolipa BA madaraka ya kuwezesha utekelezaji wa sera, malengo na programu za Umoja wa Afrika na kusimamia utekelezaji wake kikamilifu;

**LIKIZINGATIA** ripoti ya mwisho ya Kamati ya Ukaguzi na Hesabu za Umma ya Oktoba 2019, pamoja na mapendekezo yake, na maoni mbali mbali yaliyotolewa na wabunge wa BA wakati wa majadiliano kwenye Mkutano wa Bunge;

**LIKIZINGATIA KWA MASIKITIKO** kuendelea kutotekelezwa kwa mapendekezo ya ukaguzi yaliyotolewa siku za nyuma na wakaguzi wa nje, Bodi ya Wakaguzi wa Nje ya UA pamoja na Kamati ya Ukaguzi na Hesabu za Umma;

**KWA MUJIBU WA** Kanuni ya 5 (b), (c) na (d) ya Kanuni za Uendeshaji wa Bunge la Afrika, ambayo, pamoja na mambo mengine, inalipa BA mamlaka ya kuandaa mjadala, kujadili, kutoa maoni, kutoa mapendekezo na kuchukua maazimio kuhusu malengo na masuala yoyote yanayohusiana na Umoja wa Afrika na vyombo vyake, Jumuiya za Uchumi za Kanda, Nchi Wanachama na vyombo na taasisi zao;

**HIVYO LINAPENDEKEZA:**

1. Kwa UA kuzingatia Ibara ya 11(2) ya Protokali ya Mkataba Anzilishi wa Jumuiya ya Uchumi ya Afrika inayohusiana na Bunge la Afrika ya mwaka 2003 kuhusiana na bajeti ya BA na bajeti za UA kwa kuwasilisha bajeti zote za UA kwenye BA kwa ajili ya kupitiwa, kujadiliwa na kupitishwa kabla ya kuidhinishwa na Mkutano wa Wakuu wa Nchi na Serikali;

2. Kwa Vyombo vya Kisera vya UA kurudisha makato ya 50% ya bajeti kwa ajili ya bima ya matibabu ya wabunge na kuwapa wabunge wa BA hadhi, mafao na stahiki wanazostahili "Maafisa waliochaguliwa kwa mujibu wa taratibu, kanuni na sera za UA;

3. Kwa Vyombo vya Kisera vya UA kuharakisha mapitio ya viambatisho vya Makubaliano ya Nchi Mwenyeji kati ya UA na Serikali ya Afrika Kusini kuhusiana BA.

**Limepitishwa Midrand, Afrika Kusini**
**Tarehe 17 Oktoba 2019**

## PENDEKEZO LA KUTOKANA NA MKUTANO WA KUMI NA MBILI WA BUNGE LA AFRIKA KUHUSU HAKI ZA WANAWAKE

**LIKIZINGATIA** Ibara ya 17 ya Mkataba Anzilishi wa Umoja wa Afrika, ulioanzisha Bunge la Afrika ili kuhakikisha ushiriki kikamilifu wa watu wa Afrika katika maendeleo na utangamano wa kiuchumi wa bara;

**LIKIZINGATIA PIA**, Ibara ya 3 ya Protokali ya Mkataba Ulioanzisha Jumuiya ya Uchumi ya Kanda inayohusiana na Bunge la Afrika, na Kanuni ya 4 (a) ya Kanuni za Uendeshaji wa Bunge la Afrika,

**LIKIZINGATIA ZAIDI** Protokali ya Mkataba wa Afrika wa Haki za Binadamu kuhusu Haki za Wanawake katika Afrika (pia unajulikana kama Mkataba wa Maputo), Azimio Rasmi la Usawa wa Jinsia katika Afrika (SDGEA), Mkataba wa Kuondoa Aina zote za Ukatili dhidi ya Wanawake (CEDAW), Azimio la Beijing na Jukwaa la Utekelezaji na Malengo ya Maendeleo Endelevu ya Umoja wa Mataifa (SDGs) 2030, Muongo wa Wanawake Afrika (2010 – 2020), Mkakati wa UA wa Usawa wa Jinsia na Uwezeshaji wa Wanawake;

**LIKIZINGATIA** Ripoti ya Mapendekezo kutokana na Mkutano wa 12 wa haki za Wanawake uliofanywa na Bunge la Afrika tarehe 14 na 15 Oktoba 2019, Midrand, Afrika Kusini,uliokuwa na kaulimbiu ya UA ya mwaka 2019: Mwaka wa Wakimbizi, Wanaorejea Makwao na Wakimbizi wa Ndani: Kuelekea Masuluhisho ya Kudumu kwa Uhamiaji wa Kulazimishwa katika Afrika;

**LIKITAMBUA** kwamba tangu mwaka 2008 Mkutano wa Wanawake umekuwa jukwaa la kutathmini masuala ya wanawake katika Afrika na kufuatilia na kutathmini maendeleo kuendeleza haki za wanawake katika Afrika;

**LIKITAMBUA PIA** kuwa Mkutano wa Wanawake ulifanyika katika muktadha wa maadhimisho ya kumbukumbu ya miaka 50 ya kupitishwa kwa Mkataba wa Umoja wa Nchi Huru za Afrika (OAU) unaoongoza vipengele maalumu vya Wakimbizi (1969) na Kumbukumbu ya miaka 10 ya kupitishwa kwa Mkataba wa Kampala wa Wakimbizi wa Ndani (IDP);

**LIKITAMBUA KWA KUSIKITIKA** kwamba wanawake na watoto ndio wanaoathirika zaidi na migogoro na ukosefu wa makazi, na kwamba wanawake wanabeba mzigo mkubwa wa umaskini, wakipata nafasi ndogo katika michakato ya kufanya uamuzi, fedha, elimu na njia za uzalishaji;

**LIKITAMBUA PIA** kuzinduliwa kwa awamu ya operesheni ya AfCFTA tarehe 7 Julai 2019, kufuatia kuanza kutumika kwa eneo huru la biashara barani Afrika tarehe 30 Mei, 2019;

**LIKITAMBUA ZAIDI** ajenda ya UA ya 2063, ambayo inaieleza Afrika kama bara ambapo watu kusafiri kwa uhuru, kusafirisha mitaji, bidhaa na huduma kwa uhuru kutaongeza kwa kiasi kikubwa biashara na uwekezaji miongoni mwa nchi za Afrika na kuimarisha hali ya Afrika katika soko la dunia;

**LIKITAMBUA** jukumu muhimu linalofanywa na wanawake katika kutoa fursa za uzalishaji na matokeo chanya katika maendeleo ya kiuchumi na kijamii ya bara, iwe wazi au bila kutaja bayana;

**LIKITAMBUA** kwamba Wabunge, kama wawakilishi wa watu, wana wajibu mkubwa katika kujenga mazingira mazuri kwa ajili ya kutambua haki za wanawake na wasichana, ikiwa ni pamoja na kuridhia, kutumika katika nchi na kutekeleza utekelezaji wa mikataba ya kimataifa na kikanda;

**LIKITAMBUA KWA MASIKITIKO** changamoto na uchelewaji kuhusiana na kusaini, kuridhia na kutumika katika nchi kwa mikataba ya Umoja wa Afrika inayohusiana na haki za wanawake, kama vile Mkataba wa Maputo;

**KWA MUJIBU WA** Kanuni ya 5 (b), (c) na (d) ya Kanuni za Uendeshaji wa Bunge la Afrika, ambayo, pamoja na mambo mengine, inalipa BA mamlaka ya kuandaa mjadala, kujadili, kutoa maoni, kutoa mapendekezo na kuchukua maazimio kuhusu malengo na masuala yoyote yanayohusiana na Umoja wa Afrika na vyombo vyake, Jumuiya za Uchumi za Kanda, Nchi Wanachama na vyombo na taasisi zao;

SASA LINAPENDEKEZA:

1. **Kuhusu kaulimbiu ya UA kwa mwaka 2019: Mwaka wa Wakimbizi na Wakimbizi wa Ndani;**

    i. Nchi Wanachama wa UA kuweka matatizo ya wakimbizi, wakimbizi wa ndani na watu wasio na uraia katika ajenda za Baraza la Amani na Usalama la Umoja wa Afrika, Jumuiya za Uchumi za Kanda na vyombo vinavyohusika;

    ii. Nchi Wanachama wa UA kuimarisha taratibu za kina za upatanishi, kuleta amani na usuluhishi wa migogoro, ikiwa ni

pamoja na ushiriki kikamilifu wa wanawake katika shughuli na michakato yote ya kuleta amani, kufanya usuluhishaji kitaifa kupitia Muundo wa Amani na Usalama Afrika wa kulinda amani na utekelezaji na kushirikiana na mfumo wa Umoja wa Mataifa;

iii. Nchi Wanachama wa UA kutumia mbinu shirikishi na kuendeleza ushiriki wa wanawake, wakimbizi na wakimbizi wa ndani katika michakato yote ya ufanyaji uamuzi unaowaathiri

**2. Kuhusu Makubaliano ya Eneo Huru la Biashara Barani Afrika (AfCTA):**

i. Nchi Wanachama kuchukua hatua zinazofaa za kuridhia AfCTA;

ii. Nchi Wanachama kutekeleza programu za kuwawezesha wanawake kushiriki kikamilifu katika Biashara Huru na kuchagua sera zinazozingatia jinsia ili kuboresha ujumuishaji;

iii. Nchi Wanachama kuwezesha kwa makusudi wanawake kupata taarifa za biashara, huduma, fedha, TEHAMA na fursa za masoko;

iv. Wabunge wa Nchi Wanachama kufuatilia mazungumzo, utekelezaji na matokeo ya AfCTA kwa kulenga mahususi katika ushiriki wa wanawake;

v. Nchi Wanachama kujenga uwezo wa wanawake ili washiriki ipasavyo katika biashara huru na waweze kuongeza thamani katika bidhaa kwa lengo la kuongeza uzalishaji na usambazaji wa huduma.

**3. Kuhusu Muongo wa Wanawake (2010 – 2020)**

i. Nchi Wanachama kupitisha na kutekeleza kikamilifu sheria za usawa wa jinsia ambazo zinajumuisha idadi maalumu ya nafasi kwa ajili ya wanawake;

ii. Nchi Wanachama kuwasilisha ripoti zao za vipindi maalumu kuhusu Beijing +25 kwa ajili ya kupitishwa na Mawaziri wenye dhamana na Jinsia na Masuala ya Wanawake wakati wa mkutano wao utakaofanyika kuanzia tarehe 28 Oktoba hadi 1 Novemba 2019;

iii. Nchi Wanachama na Asasi za Kiraia kuandaa miradi itakayowasilishwa kwa Kamisheni ya UA ambayo itagharimiwa chini ya Mfuko kwa ajili ya Wanawake wa Afrika (FAW);

iv. Wabunge kuchukua hatua ya kushughulikia mianya iliyopo kati ya mifumo ya sera ya haki za wanawake na hali halisi ya haki za wanawake katika Afrika;

v. Wabunge wanawake kushawishi uridhiaji wa wote wa Mkataba wa Maputo ifikapo 2020 ili kutetea sera ambazo zinatoa upendeleo kwa ushirikiano wa kiuchumi wa wanawake, ujumuishaji wa jinsia katika sekta za utawala na maendeleo na uwezeshaji na ujumuishaji wa wanawake katika programu za taifa;

vi. Vyombo vya habari kuongozo kampeni za mabadiliko ya mitazamo kuhusu haki za wanawake wa Afrika kupitia uelimishaji, kuhimiza sheria, sera, na taratibu nzuri pamoja na uchunguzi na kuripoti ukatili wa kijinsia.

**4. Kuhusu Wanawake na TEHAMA**

i. Wabunge wa Afrika kuhamasisha katika Nchi zao Wanachama kupatikana kwa intaneti kama haki ya msingi.

ii. Nchi Wanachama kuhakikisha ujumuishaji wa TEHAMA katika mtaala wa shule na kuondoa vikwazo ili kuwezesha wasichana wadogo kuchukua masomo ya Sayansi, Teknolojia, Uhandisi na Hisabati (STEM).

**5. Utafutaji wa rasilimali**

i. Balozi wa Heshima wa BA wa Maendeleo ya Kiuchumi na Wanawake kutafuta rasilimali fedha zinazotakiwa kutoka katika sekta binafsi ili kusaidia:

a. Ushawishi wa utumikaji katika nchi na utekelezaji wa Mkataba wa Maputo katika nchi zote za Afrika;

b. Mawasiliano ya kimkakati katika kuhimiza kazi ya BA kuhusu haki za wanawake, hususan programu na

shughuli za Kamati ya Kundi Maalumu la Wanawake.

Limepitishwa tarehe 15 Oktoba 2019

Tarehe 17 Oktoba 2019

PAN-AFRICAN PARLIAMENT